

Ee MKATE SAFI WA UZIMA

By Sixmund J. Yumba

M/chini Parish

Agosti 2,2020

Tafakuri ya Ekaristi takatifu

Andante con anima

1. Ee - mka te sa fi wa u zi ma twa ku si fu m le ta u zi ma -
wa sta hi li si fa ya pe ke e Ee - mka te - - - - -

2. wa ro ho ya ngu - ni ka ra mu ya m fa lme m pya si ma na ya
ni pa sa ka ya she ri a m pya si ma na ya

a ga no la ka le ni ma na ya a ga no ji pya -

D.S. al fine

2. Kalvarini uliharika karamuni ulipokelewa,
umekuwa cha-kula chetu, u-mekuwa ki-nywaji chetu;
-Kwenye umbo hili la mkate,
kwenye kikombe cha di-vai, umo mzima na
Umungu wako na utukufu wako wote*2

3. Ekaristi fumbo takatifu lipitalo ufahamu wetu;
imejaa siri ilo kuu ifichikayo machoni mwetu;
-Mkate huu wa malaika; wathibitika kwa imani kuu;
ndio chakula cha wasafiri chakula cha wokovu wetu *2

4. Aulaye mwi-li- wangu na kuinywa da-mu yangu;
Hu-kaa nda-ni- yangu nami pia nda-ni- yake;
- Anilaye kwa- moyo safi; Atapata uzima milele;
anilaye bila kustahili anakula hukumu- yake *2

5. Wampokea watu kwa maelfu na wote wampokea sawa;
akipokewa hama-lizwi yumo tena ekaristini;
-Hata kipande kidogo sana; bado ni mwili wake mzima;
chakula chenye utamu mwingi chakula toka uwinguni *2

6. Ewe Kristo ulo altareni ndiwe karamu ya upendo;
umetupenda bila kifani hata kutupa mwili- wako;
-Ha-zina ya thamani kuu; Ha-zina ilo takatifu;
utukuzwe na uabudiwe siku zote hata mi-lele *2